## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI FEBRUARI, 2024 NA MWELEKEO KWA MWEZI MACHI, 2024.

**Dondoo za tathmini ya Februari, 2024 na mwelekeo wa Machi, 2024:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Februari, 2024 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Machi, 2024 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Februari, 2024 maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka yaliendelea kupata mvua za juu ya wastani pamoja na vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo na kusababisha athari ikiwemo mafuriko na uharibifu wa mali na miundombinu.


ii. Katika kipindi cha mwezi Machi 2024, mvua za msimu zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Hata hivyo, mvua za Masika zilizoanza mwishoni mwa mwezi Februari, 2024 zinatarajiwa kuendelea katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini.

iii. Joto la kawaida hadi juu kidogo ya kawaida linatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi kwa kipindi cha mwezi Machi, 2024.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2024.

Katika kipindi cha mwezi Februari, 2024 maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka yaliendelea kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi, pamoja na ongezeko la mvua kwa baadhi ya maeneo. Hata hivyo, maeneo mengi yalipata mvua za juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu wa mvua za mwezi Februari. Aidha, maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, mvua za Masika, 2024 zilianza wiki ya nne ya mwezi February, 2024 kwa maeneo mengi. Kituo cha Mahenge (Mkoa wa Morogoro) kiliripoti vipindi vingi vya mvua kubwa na kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 128.4 kilipimwa mnamo tarehe 11 Februari, 2024. Vituo vilivyopima mvua milimita 50 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1. Kwa upande mwingine, vipindi vya joto viliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini na kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 37.1°C kiliripotiwa katika kituo cha Kilimanjaro ikifuatiwa na kituo cha Moshi 36.2 °C mnamo tarehe 18 Februari, 2024.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 50 au zaidi katika mwezi Februari, 2024

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI MACHI, 2024

## 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2024, joto la Bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kati la kitropiki ya Bahari ya Pasifiki, ikiashiria kuendelea kuwepo kwa hali ya El Niño. Joto la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo kubwa la Bahari ya Hindi. Aidha, eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la juu zaidi ikilinganishwa na eneo la mashariki. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea ukanda wa pwani pamoja na mikoa ya jirani. Hali ya joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu wa kusababisha upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kuongezeka nguvu kidogo na kupelekea Ukanda mvua (ITCZ) kusogea kuelekea kaskazini.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2024

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, mvua za Masika, 2024, ambazo zimeanza mwezi Februari, 2024 zinatarajiwa kuendelea katika kipindi cha Machi, 2024. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini. Kwa upande mwingine, hali ya joto la kawaida hadi juu kidogo ya kawaida inatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo machache, hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua zinayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache hususan wiki ya kwanza ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa mnamo wiki ya kwanza ya mwezi katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Ongezeko la mvua linatarajiwa mnamo wiki ya kwanza na ya pili katika baadhi ya maeneo.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa, hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI APRILI, 2024

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2024 vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, hali ya joto la kawaida inatarajiwa katika maeneo mengi.

## 2.4 USHAURI

Mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Machi, 2024 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz